TANGAZO LA SERIKALI NA. …… la Tarehe…../…./2024

SHERIA ZA FEDHA ZA SERIKALI ZA MITAA

(SURA 290)

# SHERIA NDOGO

*Zimetungwa chini ya kifungu cha 7 (1) na 16 (1)*

## SHERIA NDOGO ZA (ADA NA USHURU) HALMASHAURI YA WILAYA YA SERENGETI ZA MWAKA 2024

## SEHEMU YA KWANZA

## UTANGULIZI

Jina na mwanzo wa kuanza kutumika

1. Sheria Ndogo hizi zitaitwa Sheria Ndogo za (Ada na Ushuru) za Halmashauri ya Wilaya ya Serengetiza toleo la mwaka 2024, na zitaanza kutumika baada ya kutangazwa katika Gazeti la Serikali.

Matumizi

2.Sheria Ndogo hizi zitatumika katika eneo lote la Mamlaka ya Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti.

Tafsiri

3.Katika Sheria Ndogo hizi isipokuwa pale itakapoelekezwa vinginevyo:-

"Ada" maana yake ni malipo yanayotozwa na Halmashauri ili kupata kibali cha kufanya shughuli yoyote ambayo kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi inastahili kulipiwa;

"Afisa Mwidhiniwa" maana yake ni mtumishi yeyote wa Halmashauri aliyeteuliwa na Mkurugenzi kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi;

"Bidhaa" maana yake ni kitu chochote kinachouzwa sokoni, gulioni, mnadani, dukani au sehemu nyingine yoyote iliyoruhusiwa;

"Chombo cha usafiri"maana yake ni chombo chochote kinachotumika kusafirisha abiria na au mizigo isipokuwa mkokoteni au wanyama;

“Halmashauri” maana yake ni Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti;

“Huduma”maana yake ni shughuli zote zinazotolewa na Halmashauri au na ambazo zinapaswakulipiwa ada na ushuru kwa mujibu wa Sheria Ndogo hizi;

“Kibali”maana yake niidhini au ruhusa ya maandishi inayotolewa na Halmashauri;

“Lori la mizigo”maanayake ni gari lolote lenye uzito kuanzia tani 3.5, ambalo hufanya kazi za kubeba mizigo, ikiwa ni pamoja na madini ya ujenzi katika eneo la Halmashauri;

“Machinjio”maana yake ni sehemu iliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuchinja wanyama, kukagua nyama na kuanika ngozi;

“Madini ya ujenzi”maana yake ni mchanga, kokoto, changarawe, mawe, kifusi na maliasili nyingine za namna hiyo ambazo kwa kawaida hutumiwa kwa ujenzi katika eneo la Halmashauri;

“Mazao” maana yake ni bidhaa zote zitokanazo na shughuli za kilimo;

“Mifugo” maana yake ni ng’ombe, mbuzi, kondoo, kuku na aina yoyote nyingine ya wanyama ambao kwa kawaida hufugwa katika eneo la Halmashauri;

“Mkurugenzi” maana yake ni Mkurugenzi Mtendaji wa Halmashauri, au Afisa yeyote wa Halmashauri anayetekeleza majukumu ya Mkurugenzi;

“Mnada” maana yake ni sehemu iliyotengwa na Halmashauri kwa ajili ya kuuza au kununua vitu mbalimbali na itajumuisha wanyama hai;

“Mnunuzi” maana yake ni mtu binafsi, taasisi au kikundi cha watu kinachojishughulisha na ununuzi wa mazao au mifugo;

“Muuzaji” maana yake ni mtu binafsi, taasisi au kikundi cha watu kinachojishughulisha na uuzaji wa mazao au mifugo;

“Soko”maana yake ni sehemu yoyote iliyotengwa na Halmashaurikwaajili ya kuuza na kununua bidhaa;

"Ushuru" maana yake ni fedha ambazo Halmashauri itatoza kwa mazao na mifugo iliyouzwa katika masoko, magulio, minada na machinjio;

"Usajili wa vyombo vya usafiri" maana yake ni utaratibu utakaowekwa na Halmashauri wa kuvitambua na kuviorodhesha katika daftari maalumndani ya Halmashauri;

"Wakala" maana yake ni mtu, taasisi,kampuni au asasi yoyote iliyoteuliwa kisheria na Halmashauri kukusanya mapato kwa niaba ya Halmashauri.

## SEHEMU YA PILI
## NAMNA YA KUKUSANYA ADA NA USHURU

Malipo ya Ada na Ushuru

4.-(1) Halmashauri itatoza Ada au Ushuru mbalimbali kwa ajili ya vibali, leseni na huduma zitolewazo na Halmashauri kama inavyooneshwa katika Jedwali la kwanza la Sheria Ndogo hizi.

(2) Ada na ushuru unaotozwa chini ya Sheria Ndogo hizi utalipwa kabla au baada ya huduma kutolewa.

(3) Huduma zitakazotozwa Ada na Ushuru katika Sheria Ndogo hizi ni:-

(a) Ushuru wa mazao;

(b) Ada na tozo za leseni au vibali;

(c) Ushuru wa madini ya Ujenzi;

(d) Ushuru wa machinjio;

**(e)** Ushuru wa mifugo iliyonunuliwa mnadani.

Wajibu wa kulipa Ada na Ushuru

5.-(1) Itakuwa ni wajibu wa kila mtu anayetakiwa kulipa Ada naUshuru kuhakikisha kwamba analipa kwa viwango vilivyoainishwa katika Jedwali la kwanza la Sheria Ndogo hizi.

(2) Muda wa kukusanya Ada na Ushuru utakuwa ni kuanzia saa kumi na mbili (12:00) kamili asubuhi mpaka saa kumi na mbili (12:00) kamili jioni.

(3) Bila kuathiri masharti ya kifungu cha 5(2) cha Afisa wa Halmashauri au wakala anaweza kukusanya

Ada naUshurubaada ya muda uliotajwa hapo juu endapo atakuwa na kibali maalum kutoka kwa Mkurugenzi wa Halmashauri.

(4) Ushuru utalipwa kila siku au kwa mwezi aukwa namna yoyote ile ambayo itakubalika kulingana na makubaliano yatakayowekwa kati ya Halmashauri na mlipa Ada na Ushuru.

(5) Malipo ya Ushuru yanayotozwa kwa mujibu wa SheriaNdogo hizi yatalipwa kwa Halmashauri au wakala wake nakutolewa stakabadhi ya Halmashauri kama kielelezo cha malipoyaliyofanyika.

(6) Pasipo kuathiri masharti ya kifungu cha 5(1-5) Mtu yeyote hatapewa kibali cha kumiliki na kuendesha machimbo ya madini ya ujenzi endapo atakuwa anadaiwa fedha na Halmashauri chini ya Sheria yoyote Ndogo ya Halmashauri.

Kulipia ushuru wa madini ya ujenzi kabla ya kuyasafirisha

6(1) Kila mmiliki au dereva wa chombo cha kusafirisha madini ya ujenzi atahakikisha kuwa analipia ushuru wa madini ujenzi kabla ya kuyasafirisha kutoka mahali yanapochimbwa au kuzalishwa Kwenda kwa mtumiaji

(2) Katika kukusanya ushuru wa madini ujenzi, Halmashauri itaweka utaratibu wa kulipia ushuru wa madini ya ujenzi.

(3) Halmashauri itatumia vibandiko maalum (sticker) katika kukusanya ushuru wa madini ujenzi kama ilivyoainishwa kwenye jedwali.

**Muda wakukusanya ushuru**

7. (1) Muda wa kukusanya ushuru utakuwa ni kuanzia saa kumi na mbili asubuhi hadi saa kumi na mbili jioni

(2) Bila kujali masharti ya kifungu kidogo cha (1), Halmashauri au wakala kwa kibali maalumu kutoka kwa Mkurugenzi, anaweza kukusanya ushuru baada ya muda uliowekwa.

(3) Malipo ya ada yatafanyika kabla ya kuanza shughuli inayolipiwa ada chini ya Sheria Ndogo hii.

(4) Ushuru utakaotozwa kwa mujibu wa Sheria Ndogo hii utalipwa kwa wakati na kuzingatia kwamba:-

a) Endapo unalipwa kwa tukio, ushuru huo

utalipwa kabla ya tukio husika kuanza

b) Endapo unalipwa kwa siku, ushuru huo utalipwa mwanzoni kabla ya shughuli ya siku hiyo kuanza

c) Endapo unalipwa kila mwezi, ushuru huo utalipwa ndani ndani ya saba (7) za mwanzo wa mwezi husika.

d) Endapo unalipwa kwa robo mwaka (yaani kila baada ya miezi mitatu) utalipwa ndani ya siku kumi nan ne (14) za mwanzo war obo husika.

e) Endapo unalipwa kwa mwaka, ushuru huo utalipwa ndani ya siku ishirini na moja za mwanzo wa mwaka husika.

f) Endapo unategemea huduma au hesabu za mapato kufanyika, ushuru huo utalipwa ndani ya siku kumi na nne baada ya huduma au hesabu za mapato kufanyika.

Usimamizi wa Sheria Ndogo

7. (1) Halmashauri inaweza kufunga biashara au kusimamisha uendeshaji wa shughuli yoyote ambayo itafanyika bila ya kuwa na leseni au kibali kinachotolewa na Halmashauri.

(2) Bila kuathiri masharti ya kifungu kidogo cha (1), Halmashauri au wakala wake anaweza kukamata na kuzuia mali au bidhaa za mtu yeyote ambaye ameshindwa kulipa ushuru na atapaswa kujaza fomu maalumu kama ilivyobainishwa katika Jedwali la pili la Sheria Ndogo hii.

(3) Endapo mmiliki wa mali au bidhaa iliyokamatwa kwa mujibu wa kifungu kidogo cha (2) atashindwa kulipa ushuru anaodaiwa ndani ya siku saba kwa mali au bidhaa zinazoharibika haraka na ndani ya siku mbili kwa mali au bidhaa zinazoharibika haraka, Halmashauri, baada ya kupata amri ya Mahakama itakuwa na mamlaka ya kuuza mali au bidhaa na fedha zitakazopatikana zitarejeshwa kwa mmiliki wa mali au bidhaa hizo baada ya kutoa ushuru unaodaiwa, gharama

za ukamataji na kuhifadhi mali au bidhaa, gharama za Mahakama na gharama za mnada.

(4) Wakala hataruhusiwa kukamata mali au bidhaa bila idhiniya maandishi ya Mkurugenzi.

(5) Halmashauri haitawajibika kwa uharibifu wa mali au bidhaa zilizokamatwa chini ya kifungu hiki isipokuwa tu kama uharibifu huo utakua umesababishwa na Halmashauri au wakala.

Uteuzi wa wakala

8. Halmashauri inaweza kuteua Kampuni, Asasi au taasisi yoyote kukusanya Ushuru kwa niaba ya Halmashauri katika vyanzo vilivyokubaliwa kukusanywa na wakala.

Wajibu wa wakala

9.-(1) Wakala aliyeteuliwa chini ya Sheria Ndogo hizi atakuwa na wajibu wa.

(a) kukusanya na kupokea Ushuru katika eneo na chanzo alichopangiwa kwa viwango vilivyoainishwa chini ya Sheria Ndogo hizi;

(b) kuwasilisha makusanyo yote kwa kuzingatia masharti ya mkataba baina yake na Halmashauri;

(c) kuweka dhamana ya kusanyo la mwezi mmoja au itakavyokubalika katika mkataba kabla ya kuanza makusanyo ambapo dhamana hiyo itarejeshwa mwisho wa mkataba.

Ukusanyaji wa madeni

10.-(1) Endapo mtu yeyote aliyetakiwa kulipa Ushuru kwa huduma zitolewazo katika eneo la mamlaka ya Halmashauri na akashindwa kulipa katika muda uliopangwa, Halmashauri inaweza kukusanya ushuru huo kwa njia ya Mahakama.

(2) Pasipo kuathiri kifungu cha 9(1) Halmashauri inaweza kukamata mali za mtu yeyote au taasisi, kampuni ambayo imeshindwa kulipa Ushuru wa Halmashauri.

(3) Baada ya kipindi cha muda wa siku thelathini (30) kupita tangu kukamatwa kwa mali za mdaiwa, Halmashauri itakuwa na mamlaka ya kuziuza kwa njia ya mnada baada ya kupata idhini ya Mahakama.

(4) Endapo mali zilizokamatwa zinaweza kuharibika kwa haraka, Halmashauri itakuwa na uwezo wa kuziuza kabla hazijaharibika baada ya kupata idhini ya Mahakama.

(5) Kwa kuzingatia masharti yaliyowekwa katika kifungu kidogo cha (3) na cha (4) hapo juu, Halmashauri kabla ya kuuza mali yoyote iliyokamatwa, itatoa taarifa ya maandishi kwa mdaiwa na umma juu ya kusudio la kuuza mali hizo.

(6) Halmashauri haitawajibika kwa hasara yoyote na kwa namna yoyote ile itakayotokea ama wakati wa kukusanya madeni au kwa mali itakayo kamatwa na kushikiliwa na Halmashauri isipokuwa kama hasara hiyo itakuwa imesababishwa na mtumishi wa Halmashauri.

Usafirishaji wa mazao

11 (1) Mazao yaliyo lipiwa ushuru yanaweza kusafirishwa kutoka sehemu moja kwenda nyingine nadni ya Halmashauri au nje ya Halmashauri.

. (2) Mtu yeyote hataruhusiwa kusafirisha mazao kutoka sehemu moja kwenda nyingine kabla ya kulipia ushuru unaotakiwa kwa mujibu wa sheria ndogo hizi.

(3) Mazao yanaweza kusafirishwa kutoka sehemu moja kwenda nyingine kabla ya jua kuchomoza na baada ya jua kuzama ikiwa tu yamelipiwa ushuru.

Kukamata chombo kinachosafirisha mazao bila kulipia ushuru

12(1) Chombo kinachosafirisha mazao kutoka sehemu moja hadi nyingine bila kulipia ushuru wa mazao husika kinaweza kukamatwa na Afisa mwidhiniwa

(2) Chombo kilichokamatwa kwa kusafirisha mazao bila kulipia ushuru kinaweza kupelekwa kwenye eneo la kupaki magari la Halmashauri (yard) na kukaa hapo hadi mmiliki wa mazao atakapolipia ushuru na faini kama ilivyoainishwa katika sheria hizi ndogo.

(3) Mmiliki wa mazao au chombo kilichokamatwa kikisafirisha mazao bila kulipia ushuru atapaswa kulipia ushuru na faini ndani ya siku tatu tangu siku ya kukamatwa chombo hicho na baada ya siku tatu (3) atatozwa gharama za kutunza au kuegesha kiasi cha shilingi elfu hamsini (50,000/=) kwa siku.

(4) Gharama za kutunza au kuegesha zilizoainishwa katika kifungu kidogo cha tatu (3) haitazidi siku kumi (10).

Ukaguzi

11.-(1) Afisa mwidhiniwa au Afisa yeyote wa Halmashauri aliyeteuliwa kusimamia utekelezaji wa Sheria Ndogo hizi atakuwa na uwezo wa:-

(a) kuingia katika jengo lolote kwa lengo la kukusanya U.shuru;

(b) kumkamata bila hati na kumshtaki mtu yeyote atakayefanya biashara kwa kuuza au kununua, kutoa huduma, kusafirisha bidhaa au kufanya shughuli yoyote iliyotakiwa kulipiwa Ushuru kwa masharti ya Sheria Ndogo hizi; au

(c) kukagua eneo au chombo chochote atakachokitilia mashaka kuwa kinahifadhi au kusafirisha bidhaa au kinatumika kukwepa kulipa Ushuru.

Wajibu wa kuzingatia masharti ya Sheria Ndogo nyingine

12.Bila kuathiri wajibu wa kulipa Ada na Ushuru, mlipaji atawajibika kuzingatia masharti ya Sheria Ndogo nyingine zinazosimamia chanzo cha mapato ikiwa ni pamoja na wajibu wa kutumia stendi kwa kupakia na kushusha abiria na mizigo, kutumia machinjio, kutunza mazingira na usafi, kutotupa taka hovyo au kutokiuka masharti mengine yaliyowekwa na Sheria Ndogo za Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti.

## SEHEMU YA TATU
## MAKOSA NA ADHABU

Makosa

13.-(1) Itakuwa ni kosa chini ya Sheria Ndogo hizi iwapo mtu yeyote:-

(a) atachimba madini ya ujenzi katika maeneo ambayo hayaruhusiwi;
(b) atashindwa, atakaidi au atakataa kulipa Ada na Ushuru au kutekeleza agizo lolote alilopewa na Halmashauri kuhusiana na ulipaji wa Ada na Ushuru;
(c) atamshawishi mtu au kundi la watu kukataa au kukwepa kulipa Ada na Ushuru;
(d) atatengeneza, atatayarisha, ataidhinisha utengenezaji au atatunza nyaraka za uongo kwa nia yakujipatia manufaa yatokanayo na ukusanyaji wa Ada na Ushuru mbalimbali ndani ya Halmashauri;
(e) atatoa taarifa za uongo kwa Halmashauri au atashindwa au kutoa taarifa zitakazo hitajika na Halmashauri;
(f) atashindwa kuweka kumbukumbu, vitabu, hesabu au maelezo yoyote ambayo Halmashauri itayahitaji;

(g) atamzuia Afisa Mwidhiniwa au wakala kutekeleza majukumu yake;
(h) atatupa taka ngumu eneo ambalo halikutengwa kama jalala au atatiririsha maji taka kwenye mitaro ya maji ya mvua;
(i) hataogesha mifugo, hatachanja mifugo;
(j) atauza nyama nje ya bucha na kuuza nyama ambayo haijakaguliwa;
(k) atasafirisha mazao ambayo hayajalipiwa ushuru.
(l) atasafirisha mazao ambayo hayajalipiwa ushuru.

(2) Mtu yeyote au taasisi au kikundi kilichoteuliwa kama wakala atahesabika ametenda kosa iwapo:-

(a) atakusanya Ada na Ushuru bila kutoa stakabadhi;

(b) atajaribu au atakusanya Ada na Ushuru kwa kiwango tofauti na kilichotajwa na Sheria Ndogo hizi;

(c) atakusanya Ada na Ushuru kwa mbinu tofauti na alizoelekezwa na Halmashauri.

Adhabu

14.Mtu yeyote atakayekwenda kinyume na masharti ya Sheria Ndogo hizi atakuwa ametenda kosa na akipatikana na hatia atatozwa faini isiyopungua shilingi laki mbili (200,000/=) na isiyozidi shilingi milioni moja (1,000,000/=) au kifungo kisichopungua miezi kumi na mbili (12) na kisichozidi miezi ishirini na nne (24) au vyote viwili kwa pamoja yaani faini na kifungo.

Kufifilisha kosa

15.Mkurugenzi anaweza kumtoza mtu yeyote faini isiyopungua laki mbili (200,000/=) na isiyozidi shilingi laki tano (500,000/=) iwapo mkosaji atakiri kosa kwa maandishi na kukubali kutekeleza wajibu wake pamoja na kulipa Ada au Ushuru anaodaiwa kwa kujaza fomu maalum ambayo iko kwenye Jedwali la Pili la Sheria Ndogo hizi.

Kufuta Sheria ndogo za Ada na Ushuru

16. Sheria hizi Ndogo za Ada na Ushuru wa Huduma za 2024 zinafuta Sheria ndogo za Ada na Ushuru za Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti zilizotangazwa kupitia Gazeti la Serikali Namba ……. la 2018

JEDWALI LA KWANZA

(*Limetungwa chini ya kifungu cha 4(1)*

I. USHURU UTOKANAO NA MAZAO

| NA. | AINA YA MAZAO | KIWANGO CHA USHURU |
|---|---|---|
| 1. | Mahindi | 3% ya bei ya kununulia |
| 2. | Mtama | 3% ya bei ya kununulia |
| 3. | Ulezi | 3% ya bei ya kununulia |
| 4. | Mpunga | 3% ya bei ya kununulia |
| 5. | Maharagwe | 3% ya bei ya kununulia |
| 6. | Alizeti | 3% ya bei ya kununulia |
| 7. | Karanga | 3% ya bei ya kununulia |
| 8. | Udaga | 3% ya bei ya kununulia |
| 9. | Dengu | 3% ya bei ya kununulia |
| 10. | Nyanya | 3% ya bei ya kununulia |
| 11. | Vitunguu | 3% ya bei ya kununulia |
| 12. | Kabichi | 3% ya bei ya kununulia |
| 13. | Matikiti maji | 3% ya bei ya kununulia |
| 14. | Viazi Vitamu | 3% ya bei ya kununulia |
| 15. | Viazi mvirigo(Ulaya) | 3% ya bei ya kununulia |
| 16. | Kunde | 3% ya bei ya kununulia |
| 17. | Mihogo | 3% ya bei ya kununulia |
| 19. | Choroko | 3% ya bei ya kununulia |
| 20. | Ngano | 3% ya bei ya kununulia |
| 21. | Maparachichi | 3% ya bei ya kununulia |
| 22. | Ndizi | 3% ya bei ya kununulia |
| 23. | Magimbi | 3% ya bei ya kununulia |
| 24. | Karoti | 3% ya bei ya kununulia |
| 25. | Biriganya | 3% ya bei ya kununulia |
| 26. | Nyanya chungu | 3% ya bei ya kununulia |
| 27. | Pilipili hoho au nyinginezo | 3% ya bei ya kununulia |
| 28. | Asali | 3% ya bei ya kununulia |
| 29. | Mbaazi | 3% ya bei ya kununulia |
| 30. | Kunde | 3% ya bei ya kununulia |
| 31. | Pamba | 3% ya bei ya kununulia |
| 32. | Tumbaku | 3% ya bei ya kununulia |
| 33. | Alizeti | 3% ya bei ya kununulia |
| 34 | Mazao mengine ya chakula yatakayolimwa kwenye eneo la Halmashauri | 3% ya bei ya kununulia |

II. ADA NA TOZO ZA LESENI NAVIBALI

| NA. | AINA YA VIBALI AU LESENI | ADA |
|---|---|---|
| 1. | (i) Kibali cha kupiga disko<br>(ii) Muziki hai, kuonyesha maigizo, sarakasi, mieleka, ngumi, vichekesho, taarabu na jazi.<br>(iii) Kibali cha kuweka mnara wa simu kwa kila mnara<br>(iv) Kibali cha ujenzi makazi<br>(v) Kibali cha ujenzi wa nyumba ya biashara<br>(vi) Kibali cha kukata barabara lami<br>(vii) Changalawe<br>(viii) Vumbi<br>( ix). Kukatisha kupitisha miundombinu ya maji na umeme | i) 30,000/= kwa siku<br>ii) 50,000/= kwa siku ya tukio<br>iii) 1,000,000/= kwa mnara<br>iv) 100/= kwa mita za mraba<br>v) 250/= kwa mita za mraba<br>vi) 350,000/=<br>vii) 100,000/=<br>viii) 50,000/=<br>ix) 30,000/= |

| | | |
|---|---|---|
| 2. | Ada ya kibali cha kusafirisha taka ngumu | 200,000/= kwa mwaka |
| 3. | Ada ya maombi ya leseni ya vileo | Tshs 3000/= |
| 4. | Ada ya pombe za kigeni rejareja;<br>i) Anayotoa huduma hapohapo katika eneo la biashara.<br>ii) Anayetoa huduma kwa mtu kwaajili ya kwenda kutumia sehemu nyingine. | i) Tshs 40,000/= kwa miezi sita<br>ii) Tshs 30,000/= kwa miezi sita |
| 5. | Ada ya leseni ya pombe za kigeni | Tshs 150,000/= kwa miezi sita |
| 6. | Ada ya leseni pombe za asili;<br>i) Maeneo ya mjini<br>ii) Maeneo ya vijijini | i) Tshs 20,000/= kwa miezi sita<br>ii) Tshs 15,000/= kwa miezi sita |
| 7. | Ada ya leseni vileo kwa hoteli za kitalii | Tshs 300,000/= kwa miezi sita |
| 8. | Ada ya leseni za vileo katika kambi za kitalii;<br>i) Kambi za kudumu<br>ii) Kambi za muda | i) Tshs 300,000/= kwa miezi sita<br>ii) Tshs 150,000/= kwa miezi sita |
| 9. | Ada ya kutoa matangazo ya sauti | 10,000/= (kwa tangazo) kwa siku |

## III. USHURU WA MADINI YA UJENZI
**Chini ya kifungu cha 6(3)**

| NA. | AINA YA BIDHAA ZINAZOSAFIRISHWA | USHURU |
|---|---|---|
| 1. | Ushuru wa mchanga, mawe, kokoto na moramu kwa lori lenye ujazo wa $M^3$ 1-5 | 90,000/= kwa mwezi |
| 2. | Ushuru mchanga, mawe, kokoto na moramu ya kujengea kwa lori lenye ujazo wa $M^3$ 5.1-12 | 150,000/= kwa mwezi |
| 3. | Ushuru wa mawe, mchanga, kokoto na moramu kwa lori lenye ujazo wa $M^3$ 12 na Zaidi | 180,000/= kwa mwezi |

## IV. USHURU WA MACHINJIO

| NA. | AINA YA USHURU/ADA | | USHURU |
|---|---|---|---|
| 1. | Ushuru wa kulaza mifugo machinjioni | Ng'ombe | 1500/= kwa siku |
| | | Ng'ombe | 1,500/= kwa kila (1) atakayechinjwa |
| 2. | Ukaguzi wa nyama | Mbuzi | 800/= kwa kila (1) atakayechinjwa |
| | | Kondoo | 800/= kwa kila (1) atakayechinjwa |
| | | Nguruwe | 1000/= kwa kila (1) atakayechinjwa |
| | | | |

### V. USHURU WA MIFUGO ILIYONUNULIWA MNADANI

| NA. | AINA YA MFUGO | USHURU |
|---|---|---|
| 1. | Ng'ombe | 7,5000/= kwa kila ng'ombe |
| 2. | Mbuzi/Kondoo | 3,000/= kwa kila mbuzi/kondoo |
| 3. | Nguruwe | 3,000/= kwa kila nguruwe |
| 4. | Tenga la kuku wasiozidi 10 | 2,000/= kwa kila tenga |

### VI. USHURU WA WAFANYABIASHARA WADOGOWADOGO

| NA. | KUNDI | KIASI |
|---|---|---|
| **1.** | **Meza ndani ya soko** | **20,000/= (kwa mwezi)** |
| **2.** | **Machinga** | **20,0000/= (kwa mwezi)** |
| **3.** | **Meza za matunda nje ya soko** | **20,000/= (kwa mwezi)** |
| **4.** | **Bidhaa zingine zinazopangwa chini nje ya soko** | **500/= (kwa siku)** |
| **5.** | **Kibanda pacha** | **30,000/= (kwa mwezi)** |
| | | |

### VII. ADA YA VIBALI KWA SHUGHULI ZA MICHEZO NA BURUDANI

| S/NO | AINA YA SHUGHULI/BIASHARA | ADA |
|---|---|---|
| 1 | Kuendesha ligi | **30,000/=** |
| 2 | Kufanya shughuli za upambaji kumbi za sherehe, mikutano na matamasha | **10,000/= kwa tukio** |
| 3 | Kuendesha kumbi za video, au banda umiza | **50,000/= kwa mwaka** |
| 4 | Biashara ya muziki wa kompyuta | **20,000/= kwa mwaka** |
| 5 | Kibali cha kuendesha michezo ya Bahati nasibu | **20,000/= kwa mwaka** |
| 6 | Play station | **50,000/= kwa mwaka** |
| 7 | Pool table | **80,000/= kwa mwaka** |
| 8 | Kibali cha muziki baani | **50,000/= kwa mwaka** |
| 9 | Kibali cha matangazo ya sauti | **20,000/= kwa siku** |
| 10 | Matangazo ya biashara | **40,000/= kwa siku** |
| 11 | Kuendesha michezo ya Marathon | **50,000/= kwa tukio** |
| 12 | Kuendesha kituo cha mazoezi ya viungo (Gym) | **50,000/= kwa mwaka** |
| 13 | Kuendesha shughuli ya MC, DJ au video shooting | **10,000/= kwa tukio.** |

**JEDWALI LA PILI**
**HATI YA KUFIFILISHA KOSA**

***(Limetungwa chini ya kifungu cha 13)***

Mimi……………………………………….………………………………………………nakiri mbele ya……………………………………………. ambaye ni Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti, kwamba mnamo tarehe……………………………..…………ya mwezi………………..mwaka………………nilitenda kosa la kukiuka masharti ya kifungu cha …………..cha Sheria Ndogo za Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti(Ada na Ushuru ) za mwaka 2024.

Kwa mamlaka aliyopewa Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti, kwa hiari yangu niko tayari kulipa kiasi cha Ada/ Ushuru unaodaiwa pamoja na faini.
Nathibitisha kuwa maelezo niliyotoa hapo juu ni ya kweli na nimeyatoa kwa hiari yangu na ufahamu wangu.

Leo tarehe…………………………… ya mwezi……………………………mwaka ………………
Jina……………………………………………………………………………………………………
Saini……………………………………………………………………………………………………
Mbele ya
Jina……………………………………………………………………………………………………
Saini……………………………………………………………………………………………………
Cheo……………………………………………………………………………………………………

Nembo ya Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti imebandikwa kwenye Sheria Ndogo hizi kufuatia azimio la Baraza la Madiwani lililoketi mnamo tarehe … mwezi……., 2024, nembo hiyo imebandikwa mbele ya:

……………………………………..
MAULID MADENI
*Mkurugenzi Mtendaji*
*Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti*

L.S

……………………………………….
AYOUB M. MAKURUMA,
*Mwenyekiti,*
*Halmashauri ya Wilaya ya Serengeti*

NAKUBALI,

Dodoma, ……………………

…………………………………
MOHAMED MCHENGERWA,
*Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais,*
*Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa.*